102/2

KISWAHILI

Karatasi 2

Mechi 2014

Muda: Saa 2½

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

MTIHANI WA MWIGO MDOGO 2014

LUGHA

Karatasi 2

Jibu maswali yote.

Kila swali lijibiwe katika karatasi tofauti.

## SEHEMU A: UFAHAMU

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali uliyopewa

Miaka ya zamani, kabla ya mabadiliko ya binadamu, ufanisi wa kupata chakula na mahitaji mengine ulitegemea ***ubabe*** wa mnyama au kiumbe anayehusika. Wale wanyama dhaifu ambao hawana vifua vya kuonyeshana ubabe kama wenzao walihasirika pakubwa. Maisha ya aina hii bado yangali miongoni mwa hayawani wanaoishi msituni. Huu hasa ndio msingi wa kauli ya "kanuni ya porini" hasa pale ambapo sheria haitumiki bali wenye nguvu wanaamua kutumia *kifua*. Ni nini hasa kinachoyadhibiti matendo ya binadamu na kuzima kuwapo kwa kanuni hiyo ya porini.

Jibu la swali hilo ni ***sahali*** sana: kuwepo kwa katiba ambayo huwa msingi wa kuiongoza jamii. Babu aliyependa mchezo wa maneno sana alizoea kueleza kimzaha "katiba ipo ili kudhibiti vitabu vya watu wasije wakawatimba wenzao!" Katiba ni nini?

'Katiba' hutumiwa kueleza mfumo mzima wa serikali ya nchi na hasa kanuni ambazo huunda na kudhibiti utendakazi wa serikali hiyo. Kwa msingi huu basi, katiba inakuwa kama roho ya nchi hiyo, ikiwa itakuwa mbaya basi nao utendakazi utakuwa mbaya.

Kanuni huweza kuwa na sheria ambazo hutambuliwa na mahakama ambazo zina jukumu la kuhakikisha kuwa zimetekelezwa na kufuatwa bila ya ubaguzi wala mapendeleo. Zipo kanuni zingine ambazo hutokana na maelewano, desturi, itikadi na kaida ambazo hudhibiti jamii inayohusika huwa sehemu ya haki za jamii yenyewe.

Nchi ambayo inatawaliwa kwa msingi wa katiba hujulikana kama serikali ya kikatiba.Serikali ambayo inatawaliwa kwa kutegemea katiba huheshimu sheria na kanuni zilizopo.Serikali hiyo hutumia katiba iliyopo kama msingi wa utendakazi wake na huhakikisha kuwa kila raia wa nchi hiyo anaitii na kuiheshimu katiba iliyopo. *Kibinimethali* cha serikali ya kikatiba ni *serikali ya ki-imla*. Serikali ya aina hii haiongozwi na sheria zozote bali huongozwa na matakwa na *hawaa ya nafsi* ya kiongozi mmoja au kigaro kidogo cha watu wanaomzunguka kiongozi wa aina hiyo. Katika nchi ya aina hiyo, sheria zilizopo hutumiwa kama nyenzo ya kuhalalisha udhalimu na kulilinda tabaka la viongozi na *vibaraka* wao.

Matendo ya serikali kikatiba kwa upande mwingine huongozwa na kudhibitiwa na vizuizi fulani. Vizuizi hivi hutokana na kuwako kwa sheria zinazolinda haki ya kila mmoja. Haki hizo hulinda raia wa nchi bila ya kujali rangi, jinsia, maumbile, dini, vionjo wala makazi yake. Jamii ya aina hiyo haiongozwi tena na msemo wa 'mwenye nguvu mpishe' au 'mnyonge kupata ni mwenye nguvu kupenda'. Badala yake huongozwa na msemo wa 'sheria ni msumeno hukata mbele na nyuma'. Ikiwa mwenye madaraka atakiuka sheria zilizopo, ataadhibiwa bila ya mapendeleo. Mnyonge naye akikiuka sheria, ataadhibiwa vivyo hivyo.

Hapo kabla tulilinganisha katiba ya nchi na roho ya nchi hiyo. Nchi ambayo haina roho ni nchi iliyokufa na isiyotegemewa kuwa na uhai wowote. Hii ina maana kuwa ili kuwa na katiba nzuri na ya kutegemewa kuna mambo kadha ya kuzingatia. Msingi wa katiba nzuri ni ufahamu wa raia wa nchi kuwa nchi yao ina hadhi kubwa kuliko wao wenyewe . Katiba nzuri ni ile ambayo itakuwa na uwezo wa kulinda jamii hiyo kwa kipindi kirefu. Haihalisi kuwa na katiba ambayo itatumiwa kwa miaka michache kisha baadaye isiweze kufaa tena. Vivyo hivyo, ni haramu mutlaki kwa katiba kuwepo kwa muda ili kuyakidhi mahitaji ya kundi fulani la watu ambalo litakuwepo kwa muda tu. Ni misingi ipi basi muhimu katika *katiba ya aushi?*

Msingi wa kwanza na wa lazima ni uzalendo. Uzalendo unakuwa nguzo kuu tunapozungumzia katiba ya nchi fulani. Uzalendo ni hisia ya kuipenda nchi yako kwa jamii inayohusika kuiwazia katiba ambayo itaendelea kuwako kwa miaka mingi ijayo. Jamii inayoongozwa na hisia za uzalendo na utaifa haitakubali kupofushwa na tamaa za muda mfupi tu. Msingi mwingine muhimu ni utambuzi wa kuwa jamii inajumlisha watu wa kila aina na wenye tofauti anuwai. Tofauti hizi zinaweza kuwa za kirangi, kilugha, kiidadi, kielimu, kimaumbile, kiuwezo n.k. Katiba nzuri lazima itilie maanani uhalisi huo na iuakisi.

Katiba haina budi kutambua kuwa kila jamii ina historia yake na hasa utamaduni na upekee wake. Kuna baadhi ya matendo ambayo ingawa yamezoeleka kwingine ni mageni na yanatisha katika

For More Free KCSE Past Papers Visit www.freekcsepastpapers.com

utamaduni mwingine, kwa mfano, uhusiano wa kimapenzi kati ya mwanamume na mwanamume mwenzake (yaani ubasha) na kati ya mwanamke na mwanamke mwenzake (usagaji). Hamna nchi ambayo inasabihiana na nyingine katika ngazi zote. Uhalisi huu lazima uwepo katika katiba ya nchi inayohusika. Haimakiniki kufuata sheria na kanuni za *nchi* ajinabi au mataifa mengine kwa kuwa yameendelea tu. Hii haina maana kuwa jamii haiwezi kukopa mambo fulani yanayoweza kuifaidi. La hasha, inaweza. Lakini kukopa nako kunahitaji kuchuja; yapi yanafaa na yapi yanaihasiri jamii. Ni muhimu kujua kuwa kiini cha katiba yoyote ile ni uwezo wa jamii wa kujiamulia mambo yao na kuyaendesha ipasavyo. Lau sivyo tunawapa wengine nafasi ya kutumia ***vitiba*** vyao kututimba sisi.

For More Free KCSE Past Papers Visit www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

a) 'Kauli ya 'kanuni ya porini' hutumiwa kwa maana gani? (alama 1)

b) Je, katiba ni nini? (alama 2)

c) i) Je, serikali inayotegemea katiba huitwaje? (alama 2)

ii) Taja sifa tatu za serikali ya aina hiyo? (alama 3)

d) Eleza misingi ya kuwapo kwa katiba itakayokuwa kwa muda mrefu. (alama 4)

e) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika kifungu.

i) Ubabe (alama 1)

ii) Sahali (alama 1)

iii) Vitiba (alama 1)

**SEHEMU B: UFUPISHO**

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

For More Free KCSE Past papers visit www.freekcsepastpapers.com

Jamii ya leo inatawaliwa na kuendeshwa na kanuni ya maarifa. Inawezekana kusema kuwa uchumi wa jamii za leo na zijazo utategemea maarifa zaidi kuliko utakavyotegemea wenzo wowote mwingine. Utambuzi na uwezo mkubwa wa maarifa katika maisha ya binadamu ndio msingi wa watu kusema 'maarifa ni nguvu.'

Maarifa huelezwa kwa tamathali hii kutokana na uwezo wa: kuyadhibiti, kuyaendesha, kuyatawala na kuyaongoza maisha ya binadamu popote pale walipo. Mtu ambaye ameyakosa maarifa fulani huwa ameikosa nguvu hiyo muhimu na maisha yake huathirika pakubwa. Kwa msingi huu, maarifa yanaweza kuangaliwa kama utajiri mkubwa ambao binadamu anaweza kuutumia kwa faida yake au kwa faida ya wanajamii wenzake. Ukweli huu ndio unaoelezwa na methali ya Kiswahili: 'Elimu ni mali.' Elimu ni chimbuko la maarifa muhimu maishani.

Msingi wa utajiri na maendeleo ya binadamu popote alipo basi ni maarifa. Je, maarifa kwa upande wake yana sifa gani? Maarifa yenyewe hayana upinzani. Maarifa uliyo nayo huweza kuwa na watu wengine wengi pasiwe na upinzani baina yenu kwa kuwa kila mmoja ana maarifa sawa. Kila mmoja ana uhuru wa kuyatumia maarifa hayo kama chanzo cha kuyazalisha maarifa mengine. Utumiaji wa maarifa yenyewe hauyamalizi maarifa hayo. Maarifa hayawezi kugusika ingawa mtu anaweza kuyanyumbua maarifa yenyewe kwa kuyatumia kwa namna tofauti.

Maarifa huingiliana na maarifa mengine. Maarifa aliyo nayo mtu mmoja huweza kuhusishwa na maarifa aliyo nayo mtu mwingine ili kuvyaza au kuzuka na maarifa tofauti. Maarifa yanaweza kuchukuliwa na kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa namna ambavyo mtu hawezi kufanya bidhaa nyingine ile. Kwa mfano, ni muhali mtu kulalamika kuwa hawezi kutembea kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa sababu ana mzigo mzito wa maarifa kichwani.

Sifa nyingine muhimu ya maarifa ni kuwa yanaweza kuwasilishwa kwa njia za ishara au mitindo mingine ya kidhahania. Ikiwa unataka kukihamisha chombo fulani kutoka sehemu moja hadi nyingine, lazima uwazie ukubwa wake, uzito wake na labda hata umbali wa panapohusika. Maarifa huweza kubadilishwa au kugeuzwa na kuwa ishara ambazo huyafanya kuwasilishwa kwa njia nyepesi kuliko kwa mfano ikiwa mtu atayawasilisha katika muundo wa, kwa mfano, kitabu.

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

Maarifa yana sifa ya uhusianaji. Kipengele fulani cha maarifa huwa na maana kinapowekwa sambamba au kugotanishwa na kipengele kingine cha maarifa. Huo huwa muktadha mzuri wa kueleweka au kuwa na maana. Kwa mfano, neno 'mwerevu' huweza kuwa na maana kwa kuwekwa katika muktadha wa 'mjinga', 'mjanja', 'hodari' na kadhalika.

Maarifa huweza kuhifadhiwa katika nafasi ndogo sana. Suala hili linaeleweka kwa njia nyepesi tunapoangalia maarifa katika muktadha wa teknolojia. Data zinazowahusu mamilioni ya watu, ambazo zingehitaji maelfu ya maktaba na lukuki ya vitabu, huweza kuhifadhiwa kwenye kifa kidogo kinachoweza kutia mfukoni.

Maarifa hayawezi kudhibitiwa au kuzuiliwa mahali fulani yasisambae. Maarifa huenea haraka sana. Maarifa ni kitu kinachoepuka pingu za watu wanaopenda kuwadhibiti binadamu wenzao. Hata pale ambapo mfumo wa kijamii au wa kisiasa unafanya juu chini kuwadhibiti raia au watu wenyewe, ni muhali kuyadhibiti maarifa yenyewe. Inawezekana kuzidhibiti njia fulani za ueneaji wa maarifa lakini maarifa hayo yatapata upenyu wa kusambaa. Ni kweli kuwa maarifa ni nguvu inayozishinda nguvu zote.

**Maswali**

a) Fupisha aya ya pili na ya tatu (maneno 55-60) [alama 5], Utiririko alama 1

b) Kwa kutumia maneno kati ya 60-65 eleza sifa za maarifa. [alama 7], Utiririko alama 2

## SEHEMU C: MATUMIZI YA LUGHA (alama 40)

a) Eleza tofauti kati ya jozi za sauti zifuatazo (alama 2)

i) /p/ na /d/

ii) /m/ na /n/

b) Eleza dhana ya shina katika kitenzi (alama 1)

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

c) Weka shadda katika jozi ya maneno haya ili kuonyesha tofauti kimaana (alama 3)

i) Wataka kazi (wanaotafuta kazi )

ii) Wataka kazi (unataka kazi)

d) Bainisha aina ya vielezi vya namna katika sentensi zifuatazo. (alama 3)

i) Wezi waliondoka ghafla

ii) Hatutawaeleza vile wenzao walivyosema

iii) Tulisafiri Afrika kusini kwa ndege

e) Bainisha viwakilishi katika sentensi zifuatazo kisha useme ni vya aina gani? (alama 3)

i) Kwingine kumepakwa rangi nyeusi

ii) Vya bure haviko viliisha

iii) Wanne hawajawasili kwa mazoezi

f) Onyesha vivumishi katika sentensi zifuatazo kisha useme ni vya aina gani? (alama 3)

i) Wafuasi walihudhuria mkutano wa kisiasa wa chama chao.

ii) Mwalimu msichana aliwanasihi wasichana

iii) Ngozi zizi hizi ndizo zenye thamani kubwa.

g) Tunga sentensi ukitumia vihisishi vifuatavyo. (alama 2)

i) Kefle

ii) Maskini

h) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya mshale. (alama 3)

Runinga iliyowachochea raia imefungwa

i) Tambua dhana zilizofungiwa kwenye mabano katika sentensi zifuatazo: (alama 3)

i) Wafanyikazi ambao wamefutwa ni wale (Kiima)

ii) Abdalla amemjengea mkewe nyumba (Shamirisho kitondo)

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

iii) Mwalimu alimchapa motto mara tatu (Chagizo)

j) Ainisha mofimu katika maneno yafuatayo. (alama 4)

i) Uendako

ii) Hataenda

k) Badilisha sentensi zifuatazo kulingana na maagizo. (alama 4)

i) Mvuvi alichoka sana (wakati ujao hali timilifu)

ii) Mtoto anafagia ukumbi wa mkutano (wakati uliopita hali ya kuendelea)

l) Tunga sentensi ukitumia vitenzi vya silabi moja. (alama 4)

i) Ja - Kauli ya kutendea

ii) Fa - Kauli ya kufanyiza

m) Tunga sentensi ukitumia viunganishi vifuatavyo. (alama2)

i) Minghairi ya

ii) Ilimradi

n) Andika sentensi zifuatazo katika usemi wa taarifa. (alama 4)

i) Ala! Wanitania nini? Mama akamwambia mwanawe

ii) "Sina la kusema sasa" Nyanya akawaambia wajukuu wake.

## SEHEMU D: ISIMU JAMII

"Mheshimiwa spika, naomba nipewe fursa kutoa maoni yangu kuhusu hoja iliyowasilishwa bungeni na mbunge wa Malishoni Mheshimiwa Potelea Mbali.........."

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

Maswali

a) Je, mazungumzo haya yanaweza kupatikana katika mazingira gani? (alama2)

b) Taja sifa zinazohusishwa na mazingira hayo zinazopatikana katika kifungu ulichosoma (alama 2)

c) Taja sifa nyingine TATU ambazo hazipatikani katika kifungu hiki. (alama 6)